



**LOWELL PUBLIC SCHOOLS**  
Ofisi za Usimamizi wa Kati Henry J. Mroz  
155 Merrimack Street  
Lowell, MA 01852

Aprili 1, 2021

Wapenzi Wanafunzi, Familia na Wafanyikazi wa Lowell Public Schools,

Tunaongojea Jumatatu hii kwa hamu, wakati ambapo wanafunzi zaidi wa madarasa ya Chekechea hadi madarasa ya 5 watarejelea masomo ya kuhudhuria darasani kibinafsi. Asante sana kwa ushiriki wenu wote, utegemezi na maoni yenu tulipokuwa tukitayarisha shule zetu kwa siku ambayo itakuwa siku ya kwanza shuleni kwa wanafunzi kadhaa katika mwaka mzima.

Bila shaka Jumatatu itakuwa siku ya kusisimua. Ili kuwasaidia mafamilia katika muda huu wa kuhamia upya katika mfumo wa masomo darasani, tumetayarisha orodha ya taarifa mpya na kumbukumbu, zikiwamo taarifa kuhusu usafirishaji, huduma ya chakula, programu yetu ya kipimo ya kikundi ya COVID-19, na taratibu zingine za usalama tunazotekeleza. Tafadhali chunguza rasilimali hizi za taarifa zilizochapishwa katika tovuti la Wilaya: <https://www.lowell.k12.ma.us/inpersonlearning>

Ingawa msisimko unaongezeka kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi inayopanuliwa, iwapo wewe ni familia ambayo inachagua kuendelea na mafunzo ya mbali hadi mwisho wa mwaka wa shule huu, tafadhali fahamu kwamba tunajitolea kulinda ubora wa mazingira ya mafunzo ya mbali. Walimu wetu na wafanyikazi wetu wa utegemezi wamekuwa wakishiriki katika mazoezi ya ziada huku wakijitayarisha kukabiliana na wanafunzi wa mbali na wa kuhudhuria madarasani wote katika wakati moja kuanzia. Na tumeweka kipaumbele uthabiti na uendelevu katika orodha za darasa ili kulinda uhusiano ambazo walimu na wanafunzi walijenga tangu mwanzo wa mwaka kadiri iwezekanavyo.

Ningependa kuwashukuru tena kwa ushiriki wenu unaoendelea, subira, urahisi wa kubadili jadwali zenu na ufahamu wenu katika mchakato huu wote tunapoendelea kutoa elimu bora zaidi kwa wanafunzi wetu, bila kujali mahali. Jumatatu itakuwa siku ya kwanza ya muundo mpya ya kusoma shule si kwa wanafunzi wengi pekee, bali pia kwa wafanyikazi wetu – na tunapoingia mazingira mapya pamoja, tunajitolea kushiriki nawe kila hatua ya barabara hiyo.

Kaa salama na kwa afya. Tunaongoja Jumatatu kwa Msisimko Mkubwa!

Wako Mwaminifu,

Dr. Joel D. Boyd  
Msimamizi Mkuu wa Mashule